**HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI MHESHIMIWA JAJI DKT. ELIEZER MBUKI FELESHI (MB) KATIKA KIKAO CHA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA TAKWIMU JIJINI DODOMA MNAMO TAREHE 18 APRILI, 2023**

- **Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria,**
- **Dkt. Evaristo Emmanuel Longopa – Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,**
- **Katibu wa Baraza la Wafanyakazi,**
- **Viongozi wa TUGHE Taifa na Mkoa wa Dodoma,**
- **Afisa Kazi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu,**
- **Mwakilishi wa Baraza Kuu la Wafanyakazi Serikalini,**
- **Mwenyekiti wa TUGHE - Tawi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,**
- **Mwakilishi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka,**
- **Mwakilishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali,**
- **Wajumbe wote wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**
- **Waandishi wa Habari,**
- **Wageni Waalikwa,**
- **Mabibi na Mabwana.**

***NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.***

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**,

Awali ya yote naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika salama mahali hapa tukiwa wazima na wenye afya kwa ajili ya kushiriki katika kikao hiki muhimu cha Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**,

Kwa heshima na taadhima, nitumie nafasi hii kwa niaba ya wajumbe wa Baraza na wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kukushukuru kukubali tena kuja kutufungulia kikao hiki cha Baraza la wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tunatambua majukumu mengi uliyonayo, lakini bado umeona ni muhimu kufika kulifungua Baraza hili rasmi. **Tunakukaribisha na tunakushukuru sana.**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**,

Pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kufanya kazi na wadau wengi, naomba nitoe shukrani za dhati na za kipekee kwa Wizara ya Katiba na Sheria, Mahakama ya Tanzania, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali kwa utendaji kazi na ushirikiano wa hali ya juu zinazoutoa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati wa utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**,

Nichukue pia nafasi hii kumshukuru Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Wakuu wa Divisheni na Vitengo na watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, viongozi wa TUGHE Tawi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wajumbe wa Baraza la wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutenga muda wao ili waweze kuhudhuria kikao hiki muhimu.

Aidha, shukrani za kipekee ziende kwa kamati ya maandalizi ambayo imefanya kazi kubwa ya kuandaa kikao hiki cha Baraza la wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia natoa pongezi kwa Baraza hili kutuchagulia Katibu na Katibu Msaidizi wa Baraza letu.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**,

Kwa kutambua umuhimu wa Baraza la wafanyakazi katika sehemu za kazi na ili kukidhi matakwa ya sheria za kazi na kutekeleza Tamko la Rais, Tamko Na. 1 la mwaka 1970 ambalo linahimiza ushirikishwaji wa wafanyakazi katika kufanya maamuzi mbalimbali ya Taasisi kupitia mabaraza ya wafanyakazi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekuwa ikifanya vikao vya Baraza la Wafanyakazi kila mwaka.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Dhumuni la kikao hiki cha Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni **kupokea na kujadili Taarifa ya Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.**

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 maeneo yafuatayo yamepewa kipaumbele kwenye bajeti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuishauri Serikali kuhusu mambo yote ya kisheria kwa kuzingatia Ibara ya 59 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 kama ilivyofanyiwa marekebisho, Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Sura ya 268, kama ilivyorekebishwa na Hati Rasmi ya Rais, Tangazo la Serikali Na. 48 la mwaka 2018:-

a) Kuandaa Toleo la Sheria Ndogo zilizorekebishwa la Mwaka 2023 zinazokadiriwa kuwa 18,000;

b) Kuandaa na kutekeleza Programu ya Elimu kwa Umma kuhusu Sheria na Haki;

c) Kuboresha Mfumo wa *Office of the Attorney General Management of Information System (OAG–MIS)* Awamu ya Tatu kwa kuanzisha moduli mpya za *e-Contracts, e-Library, e-Vetting* na *Archives;*

d) Kuwajengea uwezo watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwapatia mafunzo katika maeneo mbalimbali ikiwemo Mikataba, Uandishi wa Sheria, Ushauri wa Kisheria, Uchumi, Fedha na Utawala;

e) Uendeshaji wa Shughuli za Chama cha Mawakili wa Serikali *(Public Bar Association)*;

f) Kuendeleza ujenzi wa Vituo Jumuishi vya Taasisi za Kisheria *(Government Legal Institutions Integrated Centers-GLIICs)* katika Mkoa wa Mwanza na Arusha;

g) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji huduma za kisheria;

h) Kuendesha, kusimamia na au kushiriki katika majadiliano;

i) Kuendesha mashauri ya madai na jinai mahakamani;

j) Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utendaji kazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

k) Kuboresha maslahi ya watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

l) Ununuzi wa vitendea kazi; na

m) Kushiriki katika vikao vya Kikanda na Kimataifa.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Baada ya Baraza hili kufunguliwa rasmi, Taarifa ya Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itasomwa kwa wajumbe wa Baraza. Baada ya wasilisho hilo, wajumbe wa Baraza watapata fursa ya kujadili na kuishauri Menejimenti namna bora ya kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kukabiliana na changamoto mbalimbali zilizopo na zinazoweza kujitokeza.

Pia, wajumbe wa Baraza la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali watapitia utekelezaji wa masuala yote yaliyojadiliwa na kuwekewa maazimio katika Baraza lililopita na kujadili maslahi ya watumishi na utendaji wao wa kazi wa kila siku na namna ya kuuboresha.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Baada ya kusema hayo, naomba nitumie nafasi hii kuwaeleza wajumbe wa Bazara la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mambo mbalimbali ambayo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanikiwa kuyatekeleza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 na 2022/2023:-

**1) Ajira**

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanikiwa kuajiri watumishi wapya **50** ambapo watumishi **48** ni Mawakili wa Serikali na watumishi wawili **(2)** ni Maafisa TEHAMA, aidha mtumishi mmoja **(1)** amerejeshwa kazini.

Kabla ya mwezi Julai, 2023 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inatarajia kuajiri watumishi wapatao **13**. Hata hivyo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inapaswa kuwa na watumishi **477** na sasa ina jumla ya watumishi **182** ambayo ni sawa na **38%**, hivyo bado kuna upungufu wa watumishi **295**.

Hivyo, naiagiza Menejimenti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuendelea na taratibu za kuomba kibali cha kuajiri na kufanya uhamisho wa watumishi. Kwa kufanya hivyo, tutatimiza azma ya kuboresha huduma zetu katika maeneo yanayohitaji msukumo mpya ambayo ni-majadiliano na usuluhishi, usimamizi wa mikataba, uandishi na tafsiri ya sheria kuu na ndogo, mafunzo na utafiti.

**2) Vitendea kazi**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022 hadi mwezi Machi, 2023 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilipata ufadhili wa vitendea kazi vya **TEHAMA** vifuatavyo:

(a) Kompyuta Mpakato (Lenovo Thinkpad) moja **(1)**, Printa (Hp Laserjet & Pro MFP) mbili **(2)** na Kompyuta za mezani (Hp Elite) nne **(4)** kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT);

(b) Kompyuta Mpakato (Lenovo Thinkpad) nne **(4)** kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA);

(c) Kompyuta Mpakato (Lenovo Thinkpad) tano **(5)**, Kompyuta za mezani (Hp 200 G4 – ALL–IN-ONE) tano **(5)** na Printa (Hp Color Laserjet Pro M454dw) moja **(1)** kutoka Kagera Sugar (Superdoll);

(d) Kompyuta Mpakato (Lenovo Thinkpad) tatu **(3)**, Kompyuta za mezani (Hp 200 G4) kumi **(10)** na Printa (Hp Laserjet Pro M454dw) mbili **(2)** kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA);

(e) Kompyuta Mpakato (Hewlet Packard (HP) kumi **(10)** kutoka Kampuni ya *Williamson Diamond Limited*;

(f) Vishikwambi (Tablets – ZTE BLADE X10s) Hamsini **(50)** kutoka Wizara ya Elimu kupitia National Bureau of Statistics (NBS);

(g) Kompyuta Mpakato Sitini **(60)** (Hp envy) kati ya 150 ambazo zilitolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufuatia ahadi aliyoitoa siku ya Mkutano wa Chama cha Mawakili wa Serikali; na

(h) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanikiwa kununua Kompyuta za mezani (Desktop) **(4)**, Photocopy Machine Heavy Duty **(1)**, Laptop Macbook **(4)** na Laptop HP Spectre x 360 **(23)** kupitia ufadhili wa

Mradi Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania ***(Building Sustainable Anti- Corruption Action Tanzania (BSAAT)***.

Vifaa hivi ambavyo jumla yake ni laptop **110**, vishikwambi **50**, kompyuta za mezani **23**, printa **5** na mashine ya photocopy **1** vimesaidia kupunguza upungufu wa vitendea kazi kutokana na ufinyu wa bajeti na vitasaidia watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuanza kutumia mfumo wa *e-office*.

Kwa namna ya pekee na kwa naiba ya watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali  na wadau wote tajwa hapo juu kwa ujumla kwa kutambua mchango wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuchukua uamuzi wa kutupatia vitendea kazi hivyo ambavyo vitasaidia kuboresha utendaji kazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kiasi kikubwa.

**3) Muundo**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Katika kikao kilichofanyika tarehe 28 Novemba, 2022 ambacho kilihusisha menejimenti za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliazimiwa kwa kuanzia liandaliwe Andiko la kujenga hoja ya kuboresha muundo wa Ofisi hizi tatu zenye sifa na

majukumu yanayolandana ambao unapendekeza pamoja na mambo mengine kuwe na Divisheni za Utafiti na Machapisho katika kila ofisi.

Aidha, ilizimiwa kuwa vigezo vya Wakili wa Serikali Mwandamizi kuwa na utumishi mzuri kwa miaka mingi na au kuwa na shahada ya uzamili katika fani nyingine vitoshe kumstahilisha kupandishwa daraja kuwa Wakili wa Serikali Mkuu tofauti na kutakiwa lazima awe na shahada ya Uzamili katika Sheria (LL.M).

Vilevile, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilifanya mapitio ya muundo uliopo sasa na kufanya maboresho kadhaa ambayo yamezingatiwa katika Andiko ambalo limewasilishwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kuidhinishwa. Maboresho hayo ni pamoja na kurejesha katika Muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Kitengo cha Masjala ya Sheria kama ilivyokuwa zamani.

### 4) Maslahi ya Mawakili wa Serikali na Makatibu Sheria

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Katika kikao cha menejimenti za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Wakurugenzi wa Divisheni za Utawala na Rasilimali watu walielekezwa kuhakikisha utafiti wa kina unafanyika kuhusu viwango vya mishahara, motisha na maslahi ya Mawakili wa

Serikali na Makatibu Sheria kwa kuzingatia uzito na unyeti wa kazi wanazofanya na kuangalia mifano stahiki ndani na nje ya nchi.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa utafiti huo ulishafanyika na Andiko la kujenga hoja za kuboresha viwango vya mishahara, motisha na maslahi ya Mawakili wa Serikali na Makatibu Sheria limeshaandaliwa na kuwasilishwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kuchukua hatua stahiki.

**5) Mafunzo**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kufuatia maelekezo ya Menejimenti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliandaa Mpango wa Mafunzo kwa mwaka 2020/2021 hadi 2022/2023 kwa lengo la kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi na kuwajengea uwezo watumishi wote kulingana na kada zao. Kufikia sasa mawakili **11** wamepokea mafunzo ya stadi ya kazi katika eneo la mikataba kupitia Mradi wa *Africa Legal Service Facility (ASLF)*; maafisa waandamizi **57** kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wamepokea mafunzo elekezi ya kiutawala; watumishi **6** wamepokea mafuzo kupitia Mradi wa BSAAT na leo kuna mafunzo yatatolewa kwa watumishi **64** wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Aidha, pamoja na changamoto hiyo, katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya watumishi **13** wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali walipatiwa na wanaendelea kupata mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi katika fani mbalimbali ikiwemo Shahada ya Uzamili katika Sheria (LL.M), Uhasibu, *Applied Statistics*, *Information and Communication Technology (ICT)* na *Postgraduate in Legislative Drafting*. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti, wapo watumishi waliojigharamia mafunzo yao katika maeneo tofauti.

### 6) Mfumo wa OAG-MIS

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea kutumia Mfumo wake wa Taarifa ujulikanao kama *Office of the Attorney General Management of Information System (OAG–MIS)* ambao ulizinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 29 Septemba, 2022. Mfumo huu ndani yake, pamoja na taarifa zingine, inapatikana Miswada, Sheria na taarifa mbalimbali zinazohusu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Daftari lenye orodha ya Mawakili wa Serikali. Mfumo huo pia unasaidia kujua mahali walipo Mawakili wa Serikali pale wanapokuwa wanatekeleza majukumu yao nje ya Ofisi (*Staff Movement).*

Hadi kufikia tarehe 14 Aprili, 2023 Mawakili wa Serikali na Wanasheria waliopo katika utumishi wa umma **2837** ambao wamesajiliwa katika mfumo wa OAG-MIS na kutangazwa katika Gazeti la Serikali na 583B la tarehe 26 Septemba, 2022 walifanyiwa uhakiki ili kuthibitisha taarifa zao.

**7) Chama cha Mawakili wa Serikali**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Tokea Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania (Tanzania Public Bar Association - PBA) kilipozinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 29 Septemba, 2022, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na viongozi wa Chama hicho wamefanikiwa kufanya mambo yafuatayo:

a) Kukutana na uongozi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara ya Katiba na Sheria kwa ajili ya kupata maelekezo mbalimbali;
b) Kukutana na uongozi wa Chama cha Mawakili wa Kujitegemea (Tanganyika Law Society - TLS) kwa lengo la utambulisho, kuwasilisha ombi la Mawakili wa Serikali kutofutwa uanachama na kusamehewa madeni ya nyuma;
c) Tarehe 2 Februari, 2023 Chama cha Mawakili wa Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kilikamilisha usajili wa kikoa (domain) cha Chama, kimefanikiwa kufungua akaunti ya benki na Sanduku

la Posta kwa ajili ya mawasiliano. Taratibu nyingine zinaendelea kwa ajili ya kupata anuani ya barua pepe, tovuti na huduma nyingine za Chama kwa njia za kidijitali;

d) Mwezi Februari, 2023 uongozi wa Chama cha Mawakili wa Serikali ulishiriki katika Wiki ya Sheria jijini Dodoma. Pia, uongozi unaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kufanya maandalizi ya uzinduzi wa Kitaifa wa Kampeni ya *Mama Samia Legal Aid* inayotarajia kutekelezwa nchi nzima;

e) Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Chama cha Mawakili wa Serikali kimetengewa kiasi cha TZS **240,000,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake;

f) Aidha, tarehe 24 Aprili, 2023 wataalam wa TEHAMA kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, TLS na eGA watakutana kwa ajili ya kuoanisha (harmonize) mfumo wa *TLS-Wakili Data Base* na *OAG-MIS*;

g) Viongozi wa Chama cha Mawakili wa Serikali na Divisheni ya Uandishi wa Sheria wanatarajia kukutana kwa ajili ya kuandaa Kanuni za Uchaguzi wa viongozi wa Chama cha Mawakili wa Serikali, Miongozo na *Standard Operating Procedures (SOPs)*; na

h) Uongozi wa Chama cha Mawakili wa Serikali umewasilisha maombi ya kutumia jengo la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama Ofisi za Chama baada ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhamia katika jengo jipya linalojengwa baada ya kukamilika.

Hivyo, nawasihi viongozi na wajumbe wa Baraza la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali waendelee kutoa ushirikiano kwa uongozi wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania kwa lengo la kuboresha maslahi, utendaji kazi na kutatua changamoto mbalimbali za Mawakili wa Serikali na wanasheria wote katika utumishi wa umma kwa ujumla.

**8) Ujenzi wa Nyumba za Viongozi na Watumishi**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Katika kikao cha Baraza cha tarehe 22 Aprili, 2022 wajumbe walifahamishwa kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeomba kupatiwa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma eneo lenye ukubwa wa ekari 10 katika Mji wa Mtumba kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi *(Appartments)* za viongozi na watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Napenda kuchukua fursa hii kuwafahamisha kuwa eneo hilo limeshapatikana ambalo lina ukubwa wa Mita 62,395 katika Plot Na. 69 Kitalu JJ. Taratibu za malipo na umilikishaji zinaendelea kwa kushirikiana na mamlaka husika.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kwa asili na aina ya majukumu yake, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hutekeleza majukumu yake takribani kwa saa 18 hadi 24 kwa mfumo wa

mnyororo na mlingoti. Hili linatokana na sababu kubwa mbili: moja, Serikali inafanya kazi saa zote; na pili, viongozi wanaosafiri kwenda Nje ya nchi na Balozi zetu huihusisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenye majukumu yanayotekelezeka wakati huo bila kujalisha tofauti au kupishana kwa saa za kazi. Kwa hali hiyo, ni wazi kwamba matumizi ya ofisi mtandao tunayojenga hayataondoa adha kila siku watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kusafiri umbali kati ya 10KM hadi 30KM na zaidi kwenda ofisini na kurudi nyumbani. Ni makazi ya karibu na salama tu ndiyo yataondoa adha hii.

### 9) Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Mwaka 2021/2022 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliandaa Mpango wa kujenga Vituo Jumuishi vya Taasisi za Kisheria 11 kwa matumizi ya Taasisi za Kisheria za Serikali katika mikoa mbalimbali nchini. Mwaka 2022/2023 Serikali iliiidhinishia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali bajeti ya **Shilingi 4,000,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa Vituo Jumuishi vya Taasisi za Kisheria katika Mikoa ya Mwanza na Arusha ambao unaendelea. Aidha, Kiasi cha Shilingi 500,000,000 kiliidhinishwa kwa kazi za maendeleo kupitia Mradi Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania **(BSAAT)**.

Hadi kufikia sasa mradi wa Ujenzi wa Kituo Jumuishi cha Taasisi za Kisheria katika Mkoa Mwanza umefikia **59%**. Katika Mkoa wa Arusha, baada ya kusainiwa kwa Mkataba wa kazi mnamo tarehe 16 Februari, 2023, Mkandarasi SUMA JKT na Msimamizi wa Ujenzi ***(Consultant)*** ambaye ni Wakala wa Majengo **(TBA)** wamekabidhiwa rasmi eneo la kazi mnamo tarehe 15.4.2023. Aidha, ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mtumba, Dodoma umefikia **57%**.

Jitihada za Serikali kutafuta na kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa ujenzi wa majengo ya vituo jumuishi katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Tanga, Mtwara na Kilimanjaro zinaendelea kufanywa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango ukihusisha pia ujenzi utakaotekelezwa kwa fedha inayopaswa kutengwa kupitia Ofisi ya Mashtaka ya Taifa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Kwa nafasi yako wewe ni Waziri mwenye dhamana na miradi yote iliyo chini ya mafungu yote ya fedha chini ya Wizara ya Katiba na Sheria ambapo miongoni mwake ni Mradi wa GLIICs unaosimamiwa moja kwa moja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Kwa bahati nzuri, wewe pia ndiye uliweka jiwe la msingi la Kituo Jumuishi kinachojengwa katika Kiwanja kinachomilikiwa na Ofisi ya

Taifa ya Mashtaka kwa kutumia Fungu Na. 16 la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali eneo la Buswelu Jijini Mwanza mnamo tarehe 19 Novemba, 2022.

Kutokana na mahitaji yaliyokwishabainishwa na taasisi za kisheria za Serikali nakuomba usichoke kutupatia miongozo na maelekezo kuhusu utekelezaji wa miradi iliyo chini ya GLIICs ikiwa pia ni utekelezaji wa Maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya tarehe 16.9.2021 kama yalivyowasilishwa kwa maandishi na Katibu Mkuu Kiongozi.

Lengo ni kuwa na vituo jumuishi vitakavyosaidia utekelezaji wa majukumu ya taasisi zetu kwa mujibu wa Katiba na sheria, kurahisisha utendaji kazi, kuongeza ushirikiano baina ya taasisi mbalimbali zenye dhamana na masuala yanayohusu sheria, kupunguza gharama za uendeshaji wa ofisi, kutoa haki kwa wakati na kuondoa migongano ya maslahi na wadau mbalimbali. Nakuhakikishia kuwa, kama ulivyosikia taarifa za viongozi wa taasisi hao ulipokaa nao Jijini Mwanza tarehe 28.11.2022, viongozi hao pamoja na menejimenti zao wanayo dhamira ya dhati ya kusimamia maboresho yanayoendelea katika tasnia ya sheria.

**10) Usalama kazini**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea kuzingatia matakwa ya sheria, kanuni na miongozi mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa ili kuhakikisha usalama mahala pa kazi na kutoa huduma stahiki kwa watumishi wenye mahitaji maalum.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi na Wajumbe wa Mkutano wa Baraza,**

Nina imani kuwa pamoja na changamoto mbalimbali zilizopo, watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wataendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi, uadilifu, juhudi na maarifa. Hata hivyo, ninaomba nitumie fursa hii kutoa rai kwa watumishi wenzangu kuzingatia na kutekeleza yafuatayo wakati wa utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku:-

**1) Tathmini ya Utendaji kazi**

Naendelea kuwaomba Wakuu wa Divisheni na Vitengo waendelee kuwataka watumishi waliopo chini yao kuwasilisha taarifa za utendaji kazi za kila wiki kwa kuainisha kazi zilizopokelewa, zilizotekelezwa na ambazo hazijatekelezwa. Sina shaka yoyote kuwa, taarifa hizo zimeendelea kutusaidia kufanya tathmini kuhusu utendaji wetu wa kazi.

## 2) Utekelezaji wa Mitakaba

Naomba pia nirudie kuwaagiza Wakurugenzi kutoka Divisheni ya Mikataba na Divisheni ya Uratibu na Huduma za Kisheria kuhakikisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaletewa na kupokea nakala za mikataba na makubaliano ambayo Serikali imeingia kwa ajili ya kufanya tathmini ili Ofisi yangu iweze kuchukua hatua za kisheria mapema dhidi ya maafisa watakaobanika kutotekeleza matakwa ya mikataba na makubaliano hayo na kuisababishia serikali hasara au kuiingiza kwenye hatari ya kufikishwa kwenye vyombo vya maamuzi, kama ilivyoelekezwa na ofisi yetu mnamo tarehe 30.3.2022 na 7.11.2022. Aidha, wote mtakumbuka kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 29.9.2022 alitoa maelekezo yenye msisitizo wa aina yake katika jambo hili.

## 3) Matumizi ya TEHAMA

Kufuatia maelezo niliyotoa kuhusu vifaa vya TEHAMA tulivyopokea naomba watumishi wote waliopatiwa vifaa hivyo kuvitumia kwa uangalifu kama ilivyokusudiwa kwa manufaa ya Ofisi na Serikali kwa ujumla. Aidha, namshukuru Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maelekezo aliyotoa kwa kumtaka kila mtumishi aandike kifaa alichogawiwa ili kutunza kumbukumbu na kuiwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuendelea kuchukua hatua zingine stahiki ili kufikia lengo nililokwishatoa ifikapo Julai, 2023.

Kwa mara nyingine naomba Kitengo cha TEHAMA cha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kiendelee kuimarisha mifumo ya TEHAMA na miundombinu yake na kutoa mafunzo kwa watumishi kuhusu matumizi ya vifaa vya TEHAMA na mfumo wa *e-office* kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**4) Ushirikiano katika kazi**

Kama ilivyoelekezwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sura 2, Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura 268 naziomba Menejimenti za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali (RITA) kuongeza na kuimarisha ushirikiano uliopo miongoni mwa ofisi tajwa kwa upande mmoja na kati ya ofisi tajwa na - Wizara ya Katiba na Sheria, Mahakama na wadau wetu wengine. Menejimenti Jumuishi za ofisi hizi pia zisiache kukutana kila baada ya miezi mitatu kama zilivyoazimia mnamo tarehe 28.11.2022 kule Jijini Mwanza. Hatua hii itasaidia ufuatiliaji na utekelezaji wa maazimio mbalimbali yanayofikiwa kwenye vikao hivyo.

Aidha, kama nilivyosisitiza jana (17.4.2023) wakati ninafunga mafunzo elekezi ya ndani kwa maafisa waandamizi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nawaomba Mawakili wa Serikali waandamizi na maafisa waandamizi

kutoka Idara na Vitendo vyote vya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kushiriki kikamilifu kwenye jukumu la kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali wengine katika maeneo mbalimbali wakati wa utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

5) **Uendeshaji wa mashauri Mahakamani**

Napenda kurudia na kukazia maelekezo niliyotoa katika kikao cha Baraza cha tarehe 22 Aprili, 2022 kwamba Mawakili wa Serikali waendelee kutenga muda kimkakati kwenda kuendesha mashauri mahakamani ili kuongeza ujuzi, uwezo na uzoefu katika uendeshaji wa mashauri ya madai na jinai hivyo kufanya tathmini ya kweli ya ubora wa sheria zetu na mifumo yetu ya utoaji haki kwenye vyombo vya maamuzi vya ndani na nje ya nchi. Pia, nawaomba mawakili wale wanaopenda kusajiliwa kufanya kazi za waongoza majadiliano, usuluhishi, upatanishi na maridhiano chini ya Sheria ya Usuluhishi, Sura ya 15 kufuata taratibu zilizowekwa na kuwasilisha maombi yao mapema.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Ninawaahidi Viongozi wa Chama cha Wafanyakazi (TUGHE) Tawi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itatekeleza na kuzingatia mapendekezo yao yote yaliyotolewa na yatakayotolewa katika kikao hiki. Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

inaendelea kuomba kuongezewa bajeti na kuendelea kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,**

Baada ya maelezo hayo, kwa heshima na taadhima, naomba nikukaribishe tena ili uzungumze na wajumbe wa Baraza na kisha utufungulie Baraza hili la wafanyakazi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Napenda kukuhakikishia kuwa yale yote utakayoelekeza katika hotuba yako ambayo ni sehemu ya majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tutayafanyia kazi kwa wakati muafaka.

**NAWASHUKURU SANA KWA KUNISIKILIZA**
**NA SASA KARIBU SANA WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA,**
**DKT. DAMAS DANIEL NDUMBARO (MB)**